*Kioo cha Lugha* 2, 1996/97:101-110

# Nafasi ya Nyimbo za Kiswahili za Taarab Katika Jamii ya Kisasa

*Kitula King'ei**

## 1.0 Utangulizi

Fani iitwayo 'nyimbo' ni mojawapo ya tanzu maarufu katika fasihi simulizi katika tamaduni zote. Katika fasihi ya Kiswahili, utanzu wa nyimbo umeingiliana na kuathiriana sana kimuundo na kimtindo na utanzu wa 'shairi' hasa tukichukulia shairi kama fani au bahari moja katika uwanja wa sanaa ya ushairi kwa jumla Abdalla (1978:1-6). Katika karatasi hii hatutajishughulisha sana na swala la historia, ulinganifu au tofauti kati ya 'nyimbo' za taarab za Kiswahili na bahari nyingine za ushairi. Haya yameshughulikiwa na wataalam na wachambuzi wengine wa fasihi ya Kiswahili miongoni mwao akiwa Khatib (1981).

Dhamira ya makala hii ni kukadiria mchango uliofanywa na waimbaji wa nyimbo za taarab za Kiswahili katika mawasiliano hasa ya kimasimulizi. Ni imani ya mwandishi kuwa nyimbo za taarab zimetungwa na zinaendelea kutungwa na kusambazwa kama chombo cha mawasiliano kwa malengo kadha.

Kwa sababu hii, tunaweza kusema kuwa nyimbo hizi zina dhima au jukumu la kutimiza katika harakati za maendeleo ya nchi zetu sasa katika Afrika Mashariki. Jambo hili limedokezwa na Asha Malika, mwimbaji maarufu wa nyimbo hizi yapata miaka kumi iliyopita. Kulingana na Dumila (1977:21), msanii huyu ameeleza:

> Nyimbo zangu hutalii hisia za ndani za mwanadamu na mapenzi na matakwa yake. Hukitumia kipaji changu cha sauti tamu kwa manufaa ya wanadamu wote. Huitumia sauti yangu kuhimiza uzalendo kati ya wana Somalia wenzangu, Utaifa kati ya wanapwani wote wa Upwa wetu, Uafrika kati ya Waafrika wote na utu kati ya wote wanisikiao.

Jambo analosisitiza hapa Malika ni kwamba msanii wa taarab ana jukumu la kuchangia maendeleo ya taifa lake na wanadamu wote kwa jumla. Kama fani za fasihi ya maandishi, fani ya nyimbo hubuniwa, kuenezwa na

* Profesa Mshiriki, Idara ya Kiswahili na Lugha za Kiafrika, Chuo Kikuu cha Kenyatta

kuchambuliwa kijumuiya. Nyimbo hizi ni zao la falsafa, maoni, hisia na amali nyingine za jumuiya.

Jukumu la nyimbo za taarab kwa mtazamo wa kijamii huishurutisha fani hii kujihusisha kadiri ya mapito ya wakati. Kimuundo na kimaudhui, nyimbo za taarab zimebidika kukaa na kubadilika kufungamana na mabadiliko ya jamii zinamoibuka. Hii ndiyo sifa ya pekee inayoifanya fasihi simulizi kwa jumla na nyimbo za taarab hasa, kujitanzua na ile hoja isiyokuwa na mashiko inayoieleza fasihi simulizi kuwa "fasihi kongwe inayopokezwa kizazi hadi kizazi". Kama asemavyo F.E.M. Senkoro (1981:1) fasihi simulizi na fani zake zote.

> Ni sanaa hai ambayo nayo huhusika katika kanuni ya migongano na ya mwendo katika maisha ... sehemu zake zingine vikumbo na wakati na mazingira mapya zikabaki kuwa historia...

## 2.0 Mjadala

Nyimbo za taarab katika Kiswahili zina historia ndefu. Ni wazi kuwa utanzu wa 'nyimbo' kama ule wa ushairi umekita katika utamaduni asilia wa jamii zote za binadamu. Kwa hivyo nyimbo za taarab zinazoibwa kwa kutumia vyombo kadha wa kadha vya kimagharibi na kimashariki ni jambo lililotokea tu katika karne ya kumi na tisa hasa kati ya miaka ya 1870 na 1888. Nyimbo nyingi zilizotungwa kabla ya wakati huu, yamkini zimetoweka katika kumbukumbu. Lakini tunapoyachunguzwa maudhui ya nyimbo za taarab katika karne moja iliyopita tunapata ushahidi wa kutosha kuonyesha sanaa hii imehusika kiasi gani katika maswala ya jamii.

Kulingana na maoni ya M.S. Khatib, sanaa ya taarab katika Afrika ya Mashairiki imepitia hatua tatu muhimu na kila kipindi cha maendeleo yake kikiwa na athari fulani juu ya sanaa yenyewe kimaudhui. Kipindi cha kwanza ni cha kati ya mwaka 1970 na 1988 ambapo Waswahili walitunga taraab aghalabu katika majumba ya kifalme, hasa sehemu za Unguja ili kuwatumbuiza watawala na tabaka lao a kibwanyenye kwa jumla. Kipindi cha pili kati ya mwaka wa 1905 na 1920 ndipo makundi kadha huru ya watribu yalipoanza kubuniwa. Wakati huu nyimbo za taraab zilikuwa zimeigubika jamii finyu tu. Ni katika kipindi cha miaka ya 1920 na 1950 ambapo taarab ilianza kuenea kutoka visiwani na kupenya miji ya pwani ya Afrika Mashariki. Kutokea miaka ya 1960 taarabu imekuwa burudani maalum katika miji mingi ya pwani hata bara. Taarabu hivi leo imefikia Burundi na Rwanda.

Sasa turudi nyuma na kuyaangalia maudhui ya mjadala huu ambayo ni "jukumu na maendeleo" ya fasihi ya Kiswahili. Utanzu wa nyimbo kama utanzu mzima wa ushairi na mziki hauwezi kutenganishwa na maisha ya jamii nzima. Katika jamii zote ulimwenguni, sanaa huwa ni chombo kitumikizi. Kwa hivyo, nyimbo za taarab, katika utamaduni wa Waswahili kama kipengele kimojawapo cha fasihi ya Kiswahili zina nafasi na jukumu maalumu kama vile kuelemisha, na kutumbuiza nyimbo hizi za taarab zimewanda kimaudhui na kugubika vitabia na nyanja zote za maisha ya jamii zetu. Katika kiwango cha kiuchumi kwa mfano, taarab zimetungwa kuambatana na shughuli nyingi za kuzalisha mali kama vile uvuvi, uundaji wa majahazi, usagaji nafaka, uvunaji, usombaji mizigo, usasi na uganga. Isitoshe mziki wa aina hii umewahi kutumiwa tangu jadi kwa kuhimili na kueneza amali za kijamii kama vile elimu maadili na taasisi nyinginezo za kitaifa.

Matumizi makubwa ya mziki wa taarab hata hivyo ni katika mawasiliano ya kijamii. Watungaji wa taarab hutunga nyimbo zao aghalabu kutokana na msisimko wa hisia au kariha waipatayo kutokana na tajiriba zao za kimaisha. Nyimbo hizi hueleza hisia, fikira na mawazo ambayo ni mapana na marefu.

Katika kiwango cha kisanaa, nyimbo za taarab huonyesha umbuji wa kusarifu lugha, misemo na mafumbo yake ili kufinyanga mawazo mazito. Nyimbo hizi ambazo huwa na mdundo, mahadhi na lahani mbalimbali zenye kvutia masikizi, huwa na lengo la kuburudisha na papo hapo kufafanua, kueleza, kuchambua, kukashifu, kusifu na kuielekeza jamii. Katika kutekeleza wajibu huu, watungaji wa taarab ya Kiswahili hawajifungi kimaudhui bali hujaribu kutungia kila aina ya taathira ya maisha ya jamii. Kutokana na hili, tuna nyimbo za taarab zinazoeleza mapenzi, imani ya dini, sanaa ya lugha, siasa na kadhalika. Fungu kubwa la nyimbo hizi zimesarifu maudhui ya kuiadilisha jamii kwa kusifia nyendo zifuatazo na kukashifu upotovu wa nidhamu, uadilifu au. Tukiangazia macho maudhui haya ya kuadibu jamii katika nyimbo za taarab, tutagundua kwamba nyimbo hizi zimeshughulikia sana maendeleo yoyote ya umma yanayostahili kuitwa maendeleo hayana budi kuwa na msingi imara na mwelekeo ufaao wa kitabia, uadilifu wa utu. Jamii inayotawaliwa na mazingira yake na pia ujinga wa kukosa elimu ya kibinafsi na kiutu, huwa haiwezi kupata maendeleo yenye maana. Hapa tunaifasiri dhana ya maendeleo kwa upana wake wa kimaana kuwa juhudi za kuinua hali na kiwango cha maisha katika jamii nzima.

Maudhui ya nyimbo za taarab, hata pale ngoma za taarab zilipoonekana kuwa milki ya mabwanyenye, yalikuwa bado ni ya kijamii. Kwa mfano, Siti Binti Saad katika miaka ya 1920 alipokuwa anavuma kwa nyimbo za taarab hapa Afrika ya Mashariki, alifikiria juu ya tabia ya binadamu na uadilifu wake. Kulingana na S. Robert (1967:29), Siti aliimba:

Si hoja uzuri
Na sura jamali
Kuwa mtukufu
Na jadi kubeli
Hasara ya mtu
Kukosa akili.

Tangu miaka ya 1920 hadi leo nyimbo za taarab za Kiswahili zimekua kimaudhui. Katika nchi zetu za Afrika ya Mashariki, vikundi vingi maarufu vya taarab vimeenea hasa katika miji kama Lamu, Malindi, Mombasa, Tanga, Dar es Salaam na visiwani Unguja na Pemba. Taarab kama vile lugha na fasihi ya Kiswahili imekuwa ni milki ya jamii finyu ya waswahili bali ni chombo cha mawasiliano kwa jamii kubwa za maaifa yetu. Majina kama vile Asha Malika, Bibie Zuhura, Mohamed Kandoro, Zein Labdin, Juma Bhalo, Mualidi Juma, Jitu Mkali, Noor Khalifa, Zena Mahamud, Bibie Shakila na wengineo yamekuwa maarufu si Afrika Mashariki tu bali kote utamaduni wa Kiswahili ulipofikia. Nyimbo zao zimetumiwa kuenezea hisia, mawazo na maongozi mbalimbali ya kijamii.

Uwezo wa wasanii wa taarab wa kufinyanga popo la fikira katika lugha tamu ya kishairi yenye ukwasi wa tamathali za usemi, jazanda, taswira na mafumbo yaliyochama maana zenye undani, ni sifa moja kuu ya nyimbo za taarab. Si ajabu wachambuzi wengi wa fasihi simulizi ya Kiswahili ambao hawajachukua uzito wa kuitalii lugha na semi wanazotumia waimbaji wa taarab, wameangukia kufikiri, kama Khatibu (1981), kuwa taarab, huzungumzia mapenzi, uasherati na ugoni. Kwa hakika taarab, kama tanzu nyingine za fasihi simulizi hujadili matatizo ya jamii kwa jumla na hasa yale ya watu wa kawaida kwa kuelezea hisia, imani, hofu na ghamidha zao.

Kwa kuwa maudhui ya taarab yamefichika au kufungamana sana, si rahisi kuyafasiri kwa juu juu bila kuyafanyia makini. Pengine kule kuyapitia tu mara moja maudhui haya kuyahukumu kunatokana na ile dhana ya kikoloni iliyopuuza fasihi zetu simulizi kuwa hazikuwa na mawazo yoyote yenye maana na uzito, Kwa mfano, katika wimbo huu, Maulidi Juma, Mwimbaji wa Mombasa anazungumzia mapenzi na pia siasa katika fumbo moja tu.

Joka juu ya mdimu, limefanya ni makao
Lipapo halifahamu, lasema na wapitao
Wala halitaki ndimu, latisha wazitakao

*Kiitikio:*

Kuna joka la mdimu, mdimuni limetanda
Wala halitaki ndimu, Latisha wenye kutunda

Joka hili limezidi, kutesa wana adamu
Kwa hivyo hapana budi, lazima tulilaumu
Joka lafanya kusudi, wala halitaki ndimu

Wenzangu nawauliza, mnijibu kwa makini
Joka lingatukataza, tusifike mdimuni
Kisha ndimu zikioza, joka litapata nini?

Baada ya kuangalia wimbo kama huu, ni dhahiri kuwa mtribu hakuwa tu akifikiria juu ya mtu mwovu mwenye wivu, tadi au inda. Tumesikia mengi kuhusu baadhi yetu ambao licha ya kulimbikiza mali, vyeo na utukufu, wamejigunga kuwaangamiza walio chini yao. Ujumbe huu huu ndio uliomo katika lile shairi maarufu la Abdilatif Abdallah liitwalo, (1973:17) "Mnazi Vuta N'kuvute"

*ALII*
Ndugu ulo mnazini, wanitafuta balaa
Nakwambiya shuka tini, katakata wakataa
Wafanya nini masikani, mustarehe 'mekaa
Utashuka au la?

*BADI*
Mdugu tini ya mnazi, nilo juu nakujibu
Haya ni ya upuuzi, unambiyayo swahibu
Kushuka tini siwezi, pasi kujuwa sababu
Hiyo ni yangu jawabu

*ALII*
Sababu ya kuwambiya, ya kwamba ushuke tini
Ni kuwa nataka kweya, huko juu mnazi
Kwa ajili nami piya, nitunde nazi mwendani
N'shakweleza kwa nini

*BADI*

Hayo ni ya kutekesha,unambiyayo ndu zangu
Wataka niteremsha, juu yua mnazi wangu?
Wanistaajabisha, kuniamuru kwa changu
    Una kishaa mwenzangu

*ALII*

Sina kasha sinani, akili yangu kamili
Ni wewe usobaini, pale ulipo ukweli
Mnazi ni tangu lini, ukawa ni yuako mali?
    Sinitendee feeli

*BADI*

Wabobojekwa maneno, yasokuwa na maana
Ni ya kupumbavu mno, hayo uliyoyanena
Iwapo mnazi huno, si wangu; mbwa nani bwana?
    Sema nijuwe bayana

*ALII*

Mnazi ni wa shirika, mimi na wewe mwendani
Unshakuwa wataka, kunitowa shirikani?
Hilo halitatendeka, wala haliwezekani
    Sikubali abadani

**Marejeo** Katika kipindi cha baada ya 1960 na hasa baada ya 1965, swala muhimu katika mifumo ya siasa zetu ni kuhusu ugawaji wa mali na njia za kuzalisha mali pamoja na utajiri wote wa taifa. Utaratibu wa kikoloni tuliourithi wa kitabaka ulikuwa na kasoro nyingi hasa kwa vile haukutilia maanani usawa na haki katika ugawaji wa mali za jamii. Hali hii ilizaa mtafaruku wa migongano kati ya makundi mbalimbali. Jambo hili lilisababisha dhuluma na maonevu dhidi ya tabaka la wanyonge lililo na wengi miongoni mwa umma. Mgogoro huu wote haujawaepuka wasanii wetu wa taarab hata kidogo.

Kwa mfano, bibie Shakila anaikejeli hali hii ya ugomvi na ushindani kati ya wenye nguvu na uwezo. Anasema:

Najua mwanilaumu, mwenzenu kutojiunga
Nawajuza mfahamu, sababu ya kujitenga
Kinyang'ariyiro kitamu, lakini kina mtanga

*Kiiitikio:*

Nawajuza mfahamu, sababu y kujitenga
Kinyang'anyiro kitamu, lakini kina mtanga

Eni mliojitolea, mwenzenu nawashauri
Mimi singeyakimbia, mwajua yana dosari
Mambo yakung'angania, hayana mwisho mzuri

**Marejeo** Kwa mtazamo mmoja, huenda tukafikiri kwamba mwimbaji hapa anajieupusha na uhalisi wa maisha katika jamii yake. Hasa hili silo. Anachofanya ni kutoa utetezi wake dhidi ya uovu huyu wa kuwadhulumu wanyonge kwa sababu ya hali yao dhaifu. Hasemi, "Dau la mnyonge haliendi joshi au mnyonge hana haki". Bali anasema, "Dhuluma ina mwisho wake na wanyonge wana siku yao". Hajitengi na maendeleo ya jamii yake bali anajihusisha nayo. Ni kama Maulidi Juma anapoimba,

KANU ndiyo ilo unda, wanajeshi kukusanya
Ili wapate tulinda, na mengine ya kufanya
KANU ilileta tunda, la uhuru hapa Kenya.

*Kiitikio:*

KANU oh, kanu yajenga nchi

Yatupasa kujipinda, kulla tuliko mahali
Chama chetu kukilinda, kizindi kuwa adili
Ndicho chama kilounda, hii yetu sirikali

Hatusemi kwamba waimbaji hawa hukashifu ama kusifu tu kasuku. Kuna ushahidi wa kutosha kuonyesha kuwa nyimbo hizi huichambua jamii kwa jicho la undani.Hawachelei kuwaelekeza viongozi katika mapito yafaayo.Hii ndilo jukumu la kila msanii anayestahili kuitwa msanii wa kweli.Wasanii wakiwemo watribu, hufundisha jamii "sheria" zifaazo na kuzieleza katika umbuji wa lugha. Huwaadhibu wazivunjao sheria hizi kwa kuwakashifu na kuwazawadia wanaozizingatia kwa sifa. Wasanii hawa hujitwisha kujumu la kuwa 'waalimu' wa jamii zao.

Jambo lililo wazi kuwa si wasanii wote wa taarab wala si kila raia katika nchi zetu ambaye ameupata mwamko wa kihisia, kimawazo na kisiasa. Si kila mmoja awezaye kuichanganua jamii yake katika uhalisi wake na kwa njia ya kimantiki kiasi cha kubagua baina ya haki na batili, ukweli na unafiki; maneno matupu ya kidomo ladha na yale ya dhati. Fasihi isiyotimiza lengo

lake la kijamii haidumu na mara huchujwa na kutupiliwa mbali. Fasihi simulizi, hasa taarab, haiwezi kungojea wasanii wake waimarike kisiasa ndipo watekeleze wajibu unaowapasa kwa jamii zao. Wahakiki, waandishi, washairi na waimbaji pamoja na wanasanaa wengine wanawajibika kuihimili fani hii kwa kuipa nafasi katika jamii na vyombo vyote vya mawasiliano. Hili ndilo analohimiza Abdilatif Abdalla (1977), anaposema.

> Tucheze huku tapima, vyema tupime, miaka iliyosabiki
> Tujue tulipo kwama, tupatilize, na kung'oa visiki
> Tulipovuka salama, tutie shime, alo na haja
> Hachoki.

Mchezo unaohimizwa hapa ni kule kuutoa, kuubaini na kuutetea ukweli wa mambo kama ulivyo katika jamii zetu. Waimbaji wetu wa taarab wamejaribu kwa kiasi chao kufanya hivyo. Ukweli ndio nguzo ya maendeleo ya jamii yoyote. Kama alivyosema Shaaban Robert (1968),

> Kweli itashinda namna tunavyoishi
> Kweli haihofu tisho, wala nguvu za majeshi
> La uwongolina mwisho, kweli kitu cha uashi
> Kweli itashinda kesho, kama leo haitoshi."

Lakini taarab na fasihi yote kwa jumla ina lengo au jukumu zito zaidi ya hili la kuonyesha ukweli ulivyo au kuuchora ukweli kisanaa kwa kutumia lugha inayonata. Fasihi lazima iwe na misingi ya kinadharia na itikadi. Ni lazima ichukue msimamo hasa katika jamii zenye mifumo ya kitabaka kama zetu. Fasihi ni lazima ieneze na kupigania maendeleo kwa walio wengi kwa kujaribu kuzisisimua hisia na mawazo ya hadhira yake na hasa kuziathiri fikra na vitendo vya hadhira hii kwa njia maalumu kwa kusudi la kuleta maendeleo ya kweli kwa umma wote. Iwapo wasanii wa taarab wamefikia hatua hii iwapo wameutekeleza wajibu huu ni mambo yanayohitaji utafiti zaidi. Tangu wimbo wa kwanza wa Kiswahili uitwao "Hamziya" ulioandikwa kwa hati za Kiarabu mnamo mwaka wa 1652, hadi leo, nyimbo za Kiswahili na hasa taarab zimepiga hatua kubwa na kuchangia maendeleo ya jamii zetu. Lakini hata hivyo wasanii hawa bado wana nafasi kubwa kuweza kuimarisha hadhi na wajibu wa sanaa yao hii ili iwe chombo madhubuti cha kuwasilisha mawazo ya kimaendeleo katika jamii zetu.

### 3.0 Hitimisho

Kama tanzu nyingine za fasihi simulizi, taarab haijapata kuenezwa vyema kupitia katika vyombo vyetu vya mawasiliano na elimu kama Topan (1984) alivyosema, hili ni tatizo ambalo linaweza kutinga maendeleo ya fani hii na fasihi simulizi kwa jumla. Wakati umefika ambapo hii na fasihi simulizi kwa

jumla inapaswa, kuenezwa, kufunzwa na kutafitiwa kwa undani kwa manufaa ya maendeleo ya jamii zetu kwa jumla.

Makala hii imejaribu kujadili kwa ujumla nafasi na michango ya nyimbo za taraab kama chombo cha mawasiliano katika jamii za Afrika ya Mashariki. Ingawaje sanaa hii bado imefunguka kitamaduni katika jamii ya waswahili, lakini bila shaka athari zake zimeivuka mipaka hii na zinazidi kutapakaa. Kama anavtyosisitiza Khatib (1992), kuhusu uhusiano baina ya sanaa na jamii, tunapaswa kusisitiza jambo moja. Jambo hili ni kuwa, jamii huiwekea sanaa mipaka fulani na hali kadhalika sanaa huitungia jamii 'sheria' fulani ili kuathiri vyendo zake. Basi, ni wazi kuwa, ili kuendelea, jamii na sanaa zote hutegemeana. Fasihi andishi ama simulizi kama taarab ni kipengele cha jamii. Kwa hivyo kipengele hiki kinaathiri na kuathiriwa na jamii.

Kutoka miaka ya 1870 hadi leo, bila shaka taarab ya Kiswahili imebadilika na kukua sana kimaudhui na kimtindo. Maendeleo hayo ni thibitisho la umuhimu wa utanzu hu katika jamii. Taarabu imetumika sana katika kipindi cha kuanzia 1960 kuwasilisha maudhui ya kijamii, kisiasa na pia kukuzia na kueneza fani buifuza lugha na fasihi ya Kiswahili. Watunzi wa taarab, kama wasani wote wa fasihi na muziki, sharti watafute kariha zao katika maisha ya kila siku na hasa mitindo ya matumizi ya lugha. (Wa Thiong'o 1991:149) makala ya Mlama (1980:44) yameeleza kwa undani jinsi sanaa ya taarab ilivyoweza kusaidia kukuza lugha ya Kiswahili.

Taraab itaendelea kukua na kuenea jinsi lugha na fasihi ya Kiswahili inavyoenea. Utanzu huu utaendelea kutumika katika nyanja nyingi za maisha yetu katika eneo hili yawe ni ya kitamaduni au kisiasa. Muziki wa densi na santuri wa taarab sasa ni chumo kubwa na bila shaka utazidi kuwa maarufu katika uchumi wetu vile vile.

**Marejeleo**

Abdalla, A. (1973): *Sauti ya Dhiki,* 0xford University Press, Nairobi.

–, (1977):Utangulizi wa Abdilatif Abdalla, Mhariri wa Miaka *Kumi ya Azimio la Arusha,* UKUTA, Dar es Salaam.

–, (1978):"Ushairi wa Kiswahili na Maendeleo yake 1,'na 2", Makala ya Abdilatif Abdalla, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Bakari, M. (1978): "Language and National Identity", Karatasi ya Semina, IAS, NAIROBI.

Bukenya, A. & Zirimu, P. (1976): "0racy as a Tool for African Development" Karatasi ya Semina, Makerere, Kampala.

Campbell, C.A. (1976): "An Introduction to the music of Swahili Women" Karatasi ya Semina IAS, Nairobi.

Dumila, F. (1977): "Political Music", Makala ya *Viva*.

Kabira, W. (1983): *The 0ral Artist*, H.E.B. Nairobi.

Khamis, S.A.M. (1983): "Nafasi ya Fasihi Simulizi katika jamii ya Tanzania", Katika jarida la *Mulika* nambari 15 TUKI Dar es Salaam.

Khatibu, M.S. (1981) "Taarabu ni Fasihi Simulizi?" Karatasi ya Semina, TUKI, Dar es Salaam.

–, (1992): *Taarab Zanzibar*, Tanzania Publishing House, Dar es Salaam.

King'ei, K.G. (1992): *Language, Culture and Communication: Swahili Taarab Songs in Kenya 1963-1990*, Tasnifu ya PhD, Howard University, Washington DC.

Kipury, N. (1983): 0ral Literature of the Maasai, H.E.B. Nairobi.

Mapeje, J. (1983): *0ral Poetry from Africa*, Longman, London.

Matola, M.S. (Mhar) 1966): Waimbaji wa Juzi, TUKI, Dar es Salaam.

Mlama, P.0. (1980): "Jinsi Sanaa za Maonyesho, Taarab na Senema Zinavyoweza Kusaidia Kuimarisha Lugha ya Kiswahili" Katika Lugha Yetu. TUKI, Dar es Salaam, Na. 37:44.

0mondi, W. (1984): "The Role of Music and Dance in National Development" Karatasi ya Semina, Kenyatta University, Nairobi.

p"Bitek, 0. (1986): *Artist the ruler*, H.E.B., Nairobi

Robert, S. (1968): *Masomo yenye Adili*, Nelson, Nairobi.

Senkoro,F.E.M. (1981): "Vitendawili katika jamii. Maana, Maudhui yake na Matumizi yake", TUKI, Dar es Salaam.

Shariff, I.N. (1973): *Searching For my Brother* (Mashairi ya Kiswahili) Grossman Publishers, Madison.

Topan, F. (1984): "Fasihi Simulizi kufikia mwaka 2000 A.D" Seminar ya Kiswahili, Nairobi.

Wa Thiong'o, N. (1981): *Writers in Politics*, H.E.B., Nairobi.

–, (1991): "The Language of Struggle" katika Trnasition. 0xford University Press, New York. Na. 54:149.

Zestersten, A. (Mhar) (1983): *East African Literature*, Longman, London.